

**UTARATIBU WA KUFANYA  
HIJJAH NA ‘UMRAH  
KULINGANA NA MAFUNDISHO YA  
QUR’AN NA SUNNAH**



---

**IMETAYARISHWA NA  
DR. ISLAM MUHAMMAD SALIM**

---

# Yaliyomo

Dibaji .....	i
Sehemu ya Kwanza: Utangulizi .....	1
1.1 Maana ya Hija na Hukmu Yake .....	1
1.2 Faradhi ya Hija.....	1
1.3 Sifa za Al-Hajj Al-Mabrur .....	2
1.3.1 Ikhlas .....	2
1.3.2 Kuwafikiana na Mafundisho ya Mtume ( <i>sall-Allahu ‘alaihi wasallam</i> ) .....	3
1.3.3 Kutafuta Pato la Halali.....	3
1.3.4 Kuwa na Subra .....	4
1.4 Baadhi ya Maswala Yanayohusiana na Matayarisho ya Hija .....	5
1.4.1 Hija ya Mwanamke Bila ya Mahram <sup>0</sup> .....	5
1.4.2 Kulipa Madeni Kabla ya Hija .....	6
1.5 Maana ya Nusuk na Aina Zake .....	6
1.5.1 Tamattu’ .....	6
1.5.2 Qirān. ....	7
1.5.3 Ifrād.....	7
Mlango wa Pili: Utaratibu wa ‘Umrah .....	8
1.1 Ihraam.....	8
1.2 Miqāt.....	9
1.3 Mambo yanayopendekezwa kufanywa kabla kuingia katika ihraam	10
1.3.1 Kujisafisha .....	10
1.3.2 Kujipaka Mafuta Mazuri .....	11
1.3.3 Kuvaan Nguo ya Ihraam.....	11
1.4 Kuingia katika Ihraam .....	11
1.5 Mambo yasiyofaa kufanywa na muhrim/muhrima (sehemu ya 1) ....	12
1.5.1 Yanayokatazwa kwa mume na mke.....	12
1.5.2 Yanayokatazwa kwa mume peke yake.....	13
1.5.3 Yanayokatazwa kwa mke peke yake.....	13
1.6 Mambo yasiyofaa kufanywa na muhrim/muhrima (sehemu ya 2)....	13

1.6.1	Kuwinda wanyama wa porini.....	14
1.6.2	Kuingiliana na mke .....	14
1.6.3	Kufunga ndoa.....	14
1.7	Talbiyah .....	14
1.8	Tawāf .....	15
1.9	Mambo muhimu kuhusu Twawāf: .....	18
1.9.1	Twahara.....	18
1.9.2	Shaka katika idadi .....	18
1.9.3	Dhikri.....	19
1.10	Mambo ya sunnah katika tawāf.....	19
1.10.1	Idhtibā' .....	19
1.10.2	Al-Ramal .....	19
1.11	Swala Nyuma ya Maqam Ibrahim na Maji ya Zamzam.....	20
1.12	Sa'y baina ya Swafā na Marwa .....	20
1.12.1	Mambo Muhimu Kuhusu Sa'y.....	21
1.13	Kunyoa au kupunguza nywele za kichwa .....	22
	Sehemu ya Tatu: Utaratibu wa Kufanya Hija.....	23
1.14	Siku ya Nane (Yaumut-Tarwiyah) .....	23
1.15	Siku ya Tisa (Yaumu 'Arafah) .....	24
1.15.1	Baadhi ya Makosa yanofanyika Siku ya Arafah .....	25
1.16	Kulala Muzdalifah.....	25
1.17	Ruhusa kuondoka Muzzalifa kabla ya alfajiri .....	26
1.18	Kuokota vijiwe .....	26
1.19	Siku ya Kumi (Yaumun Nahri).....	27
1.19.1	Kurusha vijiwe ( <i>Ramyu</i> ).....	27
1.19.1.1	Baadhi ya makosa katika ramyu al-jamrah .....	28
1.19.2	Kuchinja ( <i>al-Nahr</i> ) .....	29
1.19.3	Kunyoa au Kupunguza.....	29
1.19.4	Twawāf al-ifādha .....	30
1.19.5	Sa'iy al-Hija .....	30
1.20	Utaratibu wa Amali Siku ya Kumi.....	30
1.21	Kutoka katika ihraam ( <i>Tahāllu</i> ) .....	30

1.21.1	Tahallul Ndogo .....	31
1.21.2	Tahallul kubwa.....	31
1.22	Siku za Tashreeq.	31
1.23	Kurusha Vijiwe ( <i>Ramyu</i> ) .....	32
1.24	Kulala Mina.....	33
1.25	Twawāf al-Wadaa'	33
1.25.1	Baadhi ya Makosa Katika Twawāf al-Wadā .....	34
1.26	Mwenda Madina.....	34

## Dibaji

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu. Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa walimwengu, na swala na salamu zimshukie bora wa viumbe, Mtume wa mwisho, aliyetumilizwa kwa watu wote, pamoja na ahli zake na sahaba wake pia.

Baada ya haya, ninatanguliza kurasa hizi kuhusu utaratibu wa ibadah ya hija na ‘umrah kutokana na umuhimu mkubwa wa kufahamu maudhui haya hasa kwa wale wanao azimia kutekeleza ibadah hii tukufu. Ingawa kuna vitabu vingi vizuri vinavyo zungumzia maudhui haya, wengi katika Waislamu hawapati kunufaika navyo kikamilifu kwa sababu pengine ni vitabu vikubwa au vimeandikwa kwa lugha isiyo ya Kiswahili. Hivi basi, mwongozo huu unalenga kujaliza hili pengo hilo kwa kuaelimisha Waislamu hasa wale wasiyo na uwezo wa kusoma au kuelewa lugha ya Kiarabu au Kiingereza.

Nimechagua kuandika makala ambayo si marefu sana wala si mafupi, bali kati na kati kiasi cha kubainisha mambo yaliyo muhimu katika ibadah ya hija na Umrah. Nimeyagawa makala haya katika sehemu tatu: Utangulizi, ukifuatiwa na utaratibu wa kufanya ‘umrah na kumalizia na utaratibu wa kufanya hija. Nimetaja vilevile baadhi ya makosa au mambo yanayofanyika yenyе kutatiza watu au yaliyo nje ya mafundisho yetu ya Kiislamu.

Kama kawaida ya uandishi na kazi yoyote ya kibinadamu, hapana budi kutokea nuksani, kasoro au kusahau katika sehemu fulani. Pamoja na juhud za kuhakikisha kuwa makala haya yametoka kwa njia ya kuridhisha, huenda kukawa na baadhi ya ikhtilafu za maoni au rai. Katika hali hiyo, tunakuomba ewe ndugu msomaji kuwasilisha maoni au swala lolote la ki ilimu kuititia anwani iliyo hapa chini.

*Wabillahit-Tawfiq.*

Dr. Islam Muhammad Salim  
Mombasa, Kenya  
Email: [imsalim12@gmail.com](mailto:imsalim12@gmail.com)

## Sehemu ya Kwanza: Utangulizi

### 1.1 Maana ya Hija na Hukmu Yake

- Hija katika lugha ya kiarabu maana yake ni kukusudia. Katika sheria, ni kuikusudia nyumba tukufu iliyo Makka kwa ibadah. Amesema Mola mtukufu:

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنْ أَسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ

**Na kwenda kufanya hija katika nyumba (ya Makka) ni faradhi ya Mwenyezi Mungu juu ya watu, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu (Al-'Imrān: 97)**

- Uwezo katika aya hii ni kuwa mtu anamiliki mali itakayo mpeleka kufanya hija, na mali itakayo tosheleza watu wake nyumbani (wakati akiwa hija) na gharama za usafiri.
- Yule asiye na uwezo wa mali na wasila au kipando cha kumfikisha hija, basi itakuwa kwake si lazima, na akifa akiwa hajahiji atakuwa hana lawama kwa kukosa uwezo.
- Aliye na mali lakini hawezi kutekeleza hija, ana hali mbili:
  - Ikiwa kuzuizi cha kutofanya hija si kizuizi cha daima, k.m. ugonjwa unaotarajiwa kopoa, basi ataichelewesha hija mpaka atakapoweza kutimiza ibadah hiyo.
  - Ikiwa ni kizuizi kisicho tarajiwa kuondoka, k.m. ukongwe, maradhi ya kudumu milele, n.k., basi atamwakilisha mtu atakaye ifanya hija kwa niaba yake. Dalili yake ni hadithi ya Mtume (*sall-Allahu alaihi wa sallam*) alipouliwa kuhusu mkongwe asiye weza kuthubutu juu ya kipando, Je, anawajibika kuhiji? Akajibu: "Naam, mhijie babako."<sup>1</sup>

### 1.2 Faradhi ya Hija

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

- Aya ya 97 ya Surat al-'Imrān imebainisha kuwa hija ni faradhi katika Uislamu kwa yule aliye na uwezo kutekeleza. Nayo sunnah ya Mtume (*sall-Allahu alaihi wa sallam*) ikabainisha kuwa hija inawajibika mara moja pekee katika maisha, ikizidi basi hiyo ni nyongeza.<sup>1</sup>

### 1.3 Sifa za Al-Hajj Al-Mabrur

- Imekuja katika hadithi za Mtume (*sall-Allahu alaihi wa sallam*) kuwa *hajj mabrur* haina malipo isipokuwa pepo.<sup>2</sup>
- Wanazuoni wetu wakataja maana zinazokurubiana za tamko hili wengi wakisema kuwa ni hija:
  - iliyokuabaliwa au
  - isiyokuwa na madhambi ndani yake au
  - iliyotimia kwa masharti yake na sifa inayopaswa kufanywa.
- Kutohana na hadithi hii, tunafaa tujue ni zipi sifa au sharti za hajj mabrur ambayo malipo yake ni pepo. Ili tupate hajj mabrur ni dharura kuwa na sifa hizi zifuatazo:

#### 1.3.1 *Ikhlas*

- Kama ilivyo katika ibadah zote, hija pamoja na umrah zatakiwa zifanywe kwa ajili ya Allah (*subhanahu wa ta'ala*) peke yake. Mola mtukufu akasema: “*Na timizeni amali za hija na umrah kwa ajili ya Allah*” (Al-Baqarah: 196).
- Hivi basi, haitaswihi hija wala ‘umrah ya yule ambaye anakusudia kwa ibadah hiyo malengo mengine k.m. kujionyesha kwa watu, kutaka kusifiwa kuwa kila mwaka huenda hija, kufanya biashara au malengo mengine ya kilimwengu.<sup>3</sup>

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Abu Daud, Ibn Majah na Ahmad.

<sup>2</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

<sup>3</sup> Lakini hakuna ubaya kwa anayefanya ibadah ya hija na umrah kwa *ikhlas* kuchukua fursa hio pia kufanya biashara kama ilivyo katika suratul al-Hajj.

### 1.3.2 Kuwafikiana na Mafundisho ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*)

- Hii pamoja na *ikhlaas* ndio nguzo za ibadah zote anazofanya Muislamu katika maisha yake. Lau ibadah itakua na *ikhlas* ndani yake lakini haikuafikiana na maagizo ya Mtume wetu, basi haiwezi kuwa sahihi wala kukubaliwa. Ndio maana Qur'an imetuhimiza kumfuata Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) katika ibadah na mambo yetu yote.
- Ili kutilia mkazo swala hili katika hija, Mtume wetu (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) alisema akiwa amesimama katika khutbah yake ya kuaga, “na muchukue taratibu za kufanya hija kutoka kwangu, kwani huenda tusikutane tena baada ya mwaka wangu huu.”<sup>1</sup>
- Kwa hivyo sisi ambao hatukuwahi kumwona Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) akifanya ibadah ya hija na umrah inatubidi kurudi katika vitabu vya sunnah kuangalia jinsi alivyofanya ibadah hizo.
- Kuna umuhimu mkubwa kujifundisha fiqhi na utaratibu wa hija na umrah kabla ya kuingia katika ibadah hizo kiasi kinachomwezesha Muislamu kuzitekeleza. Ni sawasawa na mtu kujifundisha ibadah ya swala yeye mwenyewe kwa makini ili aweze kuitimiza ibadah hio kikamilifu inavyofaa.
- Kinyume cha maneno haya ni kuwa ibadah inayotekelawa nje ya mafundisho sahihi ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) haitambuliwi. Hadithi inasema, “Yule anayezusha (mambo yake) katika dini yetu hii yasiyo kuwemo, atarudishiwa mwenyewe.”<sup>2</sup> Kwa hivyo hapana budi kuwa ibadah hii ni lazima iambatane na mafundisho ya sunnah, la sivyo itakuwa ni ibadah isiyo na faida ndani yake, na kupoteza mali na wakati bila manufaa.

### 1.3.3 Kutafuta Pato la Halali

- Hija ni ibadah inayohitajia uwezo wa kimwili pamoja na pesa. Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu (*subhānahu wata’āla*) ni Msafi wala hakubali ispokuwa kilicho safi, ni wajib kwa Muislamu kuhakikisha kuwa pesa zake

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Muslim

<sup>2</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

anazosafiria kwa hija, au anazompa Muislamu mwenzake kuenda hija ni za halali.

- Mafundisho ya Mtume wetu (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) yanatubainishia kuwa Mola mtukufu hakubali maombi au du'a ya yule anaye pokea pato la haramu.
- Ukipishajua hivi, je waionaje hija au umrah ya Muislamu aliyekusanya pesa zake kwa njia ya haramu kama uwizi au kutoka kwenye kazi za haramu kama hongo, ulevi au riba? Je, Mungu huridhia kweli ibadah hiyo ilhali imefanywa kwa pato lisilo safi?

#### 1.3.4 Kuwa na Subra

- Sifa hii ya *hajj mabrur* inatokana na aya ya 197 katika surat-ul Baqarah:

الْحَجَّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَاتٍ ۝ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقٌ وَلَا جِدَالٌ فِي الْحَجَّ ۝ وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ يَعْلَمُهُ اللَّهُ ۝ وَتَرَوَدُوا فِي أَنَّ خَيْرَ الرَّادِ التَّقْوَىٰ ۝ وَاتَّقُونَ يَا أُولَئِكَ الْأَلْبَابِ

Hija ni miezi maalumu. Na anaye kusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayo ifanya Mwenyezi Mungu anaijua. Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu. Na nicheni Mimi, enyi wenyewe akili!

- Kujizuia kutofanya haya yaliyo tajwa katika aya hii si rahisi hasa ukizingatia zahma la watu kutoka nchi mbali mbali wanaomiminika kwa fujo katika mji mtukufu wa Makkah.
- Muislamu anayetarajia kufanya *hajj mabrūr* atakiwa kuwa na subra na upole anapokutana na misukosuko au jambo la kuudhi. Hii ni kwa sababu kila anapostahmili kutosema au kufanya mambo yasiyofaa ndio anapopata malipo makubwa. Ndipo Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) akasema: “Yule anayehiji bila ya kusema au kufanya vitendo visvyo takiwa basi hurudi kama siku aliyo zaliwa na mamake.”<sup>1</sup>

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

## 1.4 Baadhi ya Maswala Yanayohusiana na Matayarisho ya Hija

Kuna baadhi ya maswala nyeti ambayo yanafaa kujadiliwa kwa mwongozo wa Qur'an na Sunnah kabla ya matayarisho ya hija. Tunataja maswala mawili muhimu:

### 1.4.1 Hija ya Mwanamke Bila ya Mahram<sup>(1)</sup>

- Hadithi ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) imebainisha kuwa si halali kwa mwanamke anaye muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake kusafiri bila ya kuwa na mahram au mume wake.<sup>2</sup>
- Hadithi hii haikubagua mwanamke anayesafiri kutekeleza ibadah ya hija, au mwanamke mzee au hali yeoyote. Hivi basi, kila aina ya safari ya mwanamke bila ya mahram ni kukhalifu amri ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*).
- Katika hadithi nyengine, Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) kadhalika alikataza na kuharamisha safari ya mwanamke bila ya mahram. Akasimama mmoja katika Sahaba na kusema: Mimi nimejiandikisha kutoka na kikosi fulani kwa jihadi, na mke wangu ametoka kwenda hija. Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) akamwambia: “Nenda ukahiji na mkeo.”<sup>3</sup> Katika hadithi hii kuna hoja tatu muhimu:
  - i. Kwanza, Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) hakumuuliza sahaba wake, je hiyo ni hija ya faradhi au la, bali alitoa hukmu moja kwa moja.
  - ii. Pili, Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) pia hakuuliza iwapo mke huyo yupo katika msafara na wanawake wengine (*sahabiyāt*) pamoja na kwamba kulikuwa na uwezekano mkubwa wa jambo hilo.
  - iii. Tatu, Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) alimplazimisha kufuatana na mke wake katika hija ilhali jihadi nayo ni faradhi au wajib katika Uislamu kwa wanaume. Vipi Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*)

---

<sup>1</sup> Mahram ni mtu wa karibu asiyefaa kumuoaa mwanamke,k.m. baba na kaka au mumewe.

<sup>2</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

<sup>3</sup> Imepokewa na Bukhari

angeruhusu sahaba wake kutoshiriki katika jihadi iliyo faradhi kwa kitu ambacho si haramu kwa mwanamke kufanya (tukikadiria kuwa mke huyo alisafiri peke yake)?

- Kwa hivyo, kuwepo na mahram (mumewe au mume anayehusiana na mwanamke na hawezo kumuoa) ni sharti mionganoni mwa masharti ya hija ya mwanamke kuzingatia uzito wa dalili zilizolezwa na wanazuoni wala sio kufuata kauli za madhehebu maalum bila ya dalili ya kutegemeka.

#### 1.4.2 Kulipa Madeni Kabla ya Hija

- Kinyume na inavyojulikana na watu wengi, kulipa deni au mkopo si lazima kabla ya kufanya ibadah ya hija.
- Pamoja na hivi, ni aula Muislamu kuhakikisha kuwa amelipa madeni yote kabla ya kuazimia kufanya amali ya hija wala si sharti pia kutaka ruhusa ya kuhiji kutoka kwa yule anayemdai.
- Inatosha kusajili madeni hayo na kuyahifadhi kwa mtu wa karibu ili kusiwe na mushkili wowote baadaye. Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) amehimiza sana swala la kulipa madeni kiasi cha kukataa kumsalia Muislamu yoyote aliyekuwa na deni mpaka dhima yake iondoke.

#### 1.5 Maana ya Nusuk na Aina Zake

Nusuk ni aina ya ihraam anayonuia Muislamu wakati wa kutekeleza ibada ya hija. Zimegawanyika aina tatu:

##### 1.5.1 Tamattu'

- Maana yake ni kuingia katika ihraam kwa niya ya ‘umrah katika miezi ya hija.
- Anapofika Makka anatekeleza ‘umrah kikamilifu kisha anatoka katika hiyo ihraam na kusubiri siku ya kuanza hija ili aingie katika ihraam ya pili ya hija na aikimilishe mpaka mwisho.
- Anayefanya nusuk hii huitwa *mutamatti*’ na anawajibika kuchinja mnyama kama fidya inayoitwa *fidyat al-tamattu*.

- Kwa yule asiye na uwezo wa kuchinja atafunga siku kumi kwa njia ambayo itaelezwa baadaye katika makala haya.
- Hikmah ya kuchinja kwa nusuk hii ni kutoa shukrani kwa Allah (*subhanahu wata'ala*) kwa kumwezesha kutekeleza ibadah ya hija na ‘umrah katika safari moja, badala ya kufunga safari mbili mbali mbali.
- Na vilevile imeitwa *tamattu'* kwa sababu anaye fanya *nusuk* hii ana fursa ya kupumzika na kustarehe baina ya ibada ya umrah na hija. Kwa rai ya wanazuoni wengi, hii ndio *nusuk* iliyo bora kati ya hizi *nusuk* tatu.<sup>1</sup>

### 1.5.2 *Qirān*.

- Maana yake ni kuchanganya ibada ya ‘umrah na hija katika niya moja.
- Anayefanya hivi huitwa *qaarin* na amali zake za ‘umrah zinakuwa ndio hizo hizo amali za hija, kama vile twawaaf, sa’y na nyenginezo.
- Kwa anayefanya *nusuk* hii, anawajibika pia kuchinja mnyama kama ilivyo katika *tamattu'* kwa sababu ya kuchanganya ibada hizi mbili. Hii ndio *nusuk* aliyoifanya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) kwani alikuwa amemchukua mnyama wake wa kuchinja kutoka Madina.
- Na yoyote anayeingia na mnyama wa kuchinjwa kutoka nje ya *haram* ya Makka itamlazimu afanye *nusuk* ya qiraan.

### 1.5.3 *Ifrād*.

- Maana yake ni kufanya Hija peke yake, na anayefanya *nusuk* hii huitwa *mufrid*.
- Amali anazozifanya hazitofautiani na zile za *qaarin* ispokuwa katika niya na kuchinja. *Mufrid* hunuia kufanya hija pekee ilhali *qaarin* hutia niya ya umrah na hija.
- Kwa sababu hii, huyu *mufrid* hawajibiki kuchinja kwa kuwa amekusudia kufanya ibada moja peke yake.

---

<sup>1</sup> Al-Mughni: Ibn Qudamah, uk. 123

## Mlango wa Pili: Utaratibu wa ‘Umrah

- Wawakilishi wa ibadah za hija na ‘umrah huweka mpangilio fulani wa kutelekeza ibadah hizo kabla ya kuondoka nchini. Kuna aina mbili mashuhuri ya mipangilio hiyo:
  - Kuanza Makkah kwa ibadah ya ‘umrah na kumalizia kwa ziyara ya Madina:



Kupitia kwa utaratibu huu muhujaji wanawajibika kunuia ihraam ya ‘umrah wanopita katika *miqaat*<sup>4</sup> kabla ya kufika Jeddah. Baada ya kukamilisha amali ya ‘umrah, wanasubiri siku ya kuanza ibadah ya hija.

- Kuanza Madina kwa Ziyara na kumalizia Makkah:



- Kupitia kwa utaratibu huu, mahujaji hushukia Jeddah bila ya kunuia ihraam ya ‘umrah kisha wanaelekea Madina. Baada ya kukamilisha ziyara ya Madina, hunuia ‘umrah na kuvalaa ihraam kabla ya kuelekea Makkah.

### 1.1 Ihraam

- Amali ya kwanza ya hija au ‘umrah ni ihraam ambayo ni niya ya kuingia katika *nusuk*. Imeitwa ihraam kwa sababu baada ya kuingia katika ibadah ya hija au ‘umrah yanaharamishwa mambo ambayo yalikuwa ni halali kwa Muislamu.
- 

<sup>4</sup> Yatakuja maelezo yake kwa kirefu

## 1.2 Miqāt

- Niya hii ya kuingia katika ihraam imeekewa *mīqāt* (vituo vyake maalum vinavyo zunguka mji mtukufu wa Makkah). Hivi basi, haifai kuingia Makkah bila ya ihraam inayopaswa kufanywa katika vituo hivyo.
- Ramani ifuatayo inatuonyesha vituo hivi alivyo viweka Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*).



Kituo	Miqaat	Umbali kutoka Makka
Dhul Hulaifah (Abyar Ali)	Wakaazi wa Madina au wapitao hapo	410 km
Al-Juhfa (Rābigh)	Watokao Sham, Afrika kaskazini na Ulaya	203 km
Dhatu 'Irq	Watokao Iraq au wapitao hapo	88 km
Qarn al-Manazil (Al-Sail)	Watokao sehemu za Najd na Emaraat	80 km
Yalamlam	Watokao Yemen au wapitao hapo	128 km

- Kwa Waislamu watokao maeneo ya mashiriki ya Afrika (Kenya na jirani) *miqaat* yao iko Yalamlam, pia inaitwa Al-Sa'diyah umbali wa kilomita 128 kutoka mji mtukufu wa Makkah.
- Ikiwa mpangilio wa *nusuk* ni kuanza na Makkah kufanya ‘umrah kwanza, italazimika kuingia katika ihraam kabla ya kuvuka Yalamlam. Na kwa kuwa tunaipita *miqaat* hii kwa ndege tukiwa angani, inawajibika kutia niya ya kuingia katika ‘umrah tukiwa hapo angani ili tukishuka uwanja wa ndege wa Jeddah itakuwa tayari tuko ndani ya ihraam. Hii ni kwa sababu Jeddah, ambayo ipo ndani ya *miqaat*, si kituo cha kuhirimia kwa watu wanaotoka huku Afrika mashariki.
- Ikiwa mpangilio sio kuanza na ‘umrah bali ni kuelekea moja kwa moja hadi Madina, inambidi Muislamu asinuie ‘umrah anapoondoka nchini kwake. Bali anawajibika kunuia ziyara ya Masjid al-Nabawi peke yake. Baada ya kutimiza siku zake alizopanga kukaa Madina, ndio hapo atanua kufanya ‘umrah kuitia kituo cha watu wa Madina (Abyaar ‘Ali). Hapo ndipo atakapoingia katika ihraam ya kufanya ‘umrah.

### 1.3 Mambo yanayopendekezwa kufanya kabla kuingia katika ihraam

#### 1.3.1 Kujisafisha

- Utajisafisha kwa kukata kucha zilizo ndefu, masharubu, nywele za kwapani na sehemu za siri kabla ya kuoga. Na haya ni jumla ya mambo ya *fitrah* ambayo Uislamu umeyasistiza.
- Ni sunnah kwa Muislamu kukata nywele hizo na kucha angalau kila siku arbaini kama ilivyo katika hadith.<sup>1</sup>
- Baada ya hapo ataoga mwili wote na hii vile vile imependekezwa kabla ya kuingia katika ihraam.
- Hata mwanamke aliye katika ada za mwezi pia inapendekezwa kuoga kwa sababu kuoga huku ni kujisafisha wala sio kwa niya ya kujitwahirisha.

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Muslim.

### 1.3.2 Kujipaka Mafuta Mazuri

- Baada ya kujisafisha atajipaka manukato au mafuta mazuri mwilini hasa zile sehemu ambazo anataka ziwe na harufu nzuri kama kwapani. Lakini awe na tahadhari ya mambo mawili:
  - a. Asijipake mafuta katika nguo za ihraam anayoivaa, kwa sababu nguo ya ihraam haitiwi mafuta mazuri wala manukato yoyote.
  - b. Tahadhari ya pili ni mwanamke ambaye haruhusiwi kisheria kuijwekea mafuta mazuri na kupita mbele ya wanaume. Imethubutu katika hadithi za Mtume wetu (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) kuwa mwanamke anaye paka mafuta ya harufu nzuri kisha apite mbele ya wanaume wainuse harufu ile huwa ni mzinifu.<sup>1</sup> Pahali anapotakiwa mwanamke kujipaka mafuta hayo mazuri ni katika nyumba ya mumewe ambaye ni halali yake hata akiathirika na harufu hiyo.

### 1.3.3 Kuvaan Nguo ya Ihraam

- Akimaliza usafi, atavaa nguo ya ihraam ambayo kwa mwanamume ni nguo mbili: ya chini ni *izār* (huvaliwa kama kikoi au saruni) na nyengine ni *ridā* (huvaliwa sehemu ya juu ya mwili kama shuka).
- Hakuna rangi maalum kwa vazi la ihraam ispokuwa inapendekezwa kuwa ni nyuepe kwa hadithi ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) “Vaeni katika mavazi yenu yalo rangi nyeupe na muwakifini (kwa nguo za rangi hiyo) maiti zenu.”<sup>2</sup>
- Mwanamke, anaruhusiwa kuvaan nguo yoyote ya rangi yoyote, si lazima ya rangi nyeupe. Muhimu isiwe nguo ya mapambo au ya kuvutia macho.

## 1.4 Kuingia katika Ihraam

- Baada ya kujitayarisha, ataingia katika ihraam. Kwa anayefanya *nusuk* ya *tamattu*, niya yake itakuwa:
- Baada ya niya hii, atakua ameingia katika ihraam ya ‘umrah.

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Abu Daud na Al-Hakim

<sup>2</sup> Imepokewa na Al-Tirmidhi na Abu Daud

- Mara nyingi watu huswali rakaa mbili za sunnah baada ya hapo iitwayo: sunnat-ul ihraam. Hakuna dalili ya wazi kuonyesha kuwa ihraam ina swala yake makhsus. Ikiwa imekaribia swala ya faradhi, ni ubora kuichelewesha ihraam hadi kumaliza kuswali kisha anuie. Hivi ndivyo alivyofanya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*).
- Pamoja na hivi, akiswali hakuna ubaya iwapo haitaafikiana na wakati ulio katazwa kuswali.

## 1.5 Mambo yasiyofaa kufanywa na muhrim/muhrima (sehemu ya 1)

- Baada ya kunuia ihraam, kuna mambo maalum haruhusiwi muhrim (aliye katika hali ya ihraam) kuyafanya. Sehemu ya kwanza ya mambo haya ni yale ambaye fidya yake ni fidya ya udhia. Fidya hii inawajibika lau mtu atayafanya haya yaliyo katazwa kwa kujua na/au kusudi. Nayo ni:
  - kufunga siku tatu (mfululizo au kwa kukata), au
  - kulisha maskini sita kiwango cha nusu ya *sā'kila mmoja*<sup>1</sup> au
  - kuchinja mnyama (mbuzi au kondoo) na kuwapa mafakiri (bila ya kula katika nyama hiyo).
- Anayefanya moja wa haya kwa kutojua kuwa haifai au kusahau, hana lawama.

### 1.5.1 Yanayokatazwa kwa mume na mke

- Kati ya hayo, kuna mambo ambayo mume na mke wote wanashirikiana katika makatazo na hawafai kuyafanya:

---

<sup>1</sup> Kiwango cha nusu ya *sa'* ni takriban kilo moja na nusu ya mchele



Akifanya moja wapo katika hizi itamlazimu fidya:

Kufunga (Siku 3) au  
Kulisha (Maskini 6) au  
Kuchinja (Mbuzi au kondoo)

### 1.5.2 Yanayokatazwa kwa mume peke yake

- Mwanamume (Muhrim) peke yake anakatazwa kufanya haya mambo mawili:
  - a. Kufinika kichwa kwa kitu kinacho shikana na kichwa. Kwa mfano, kofia, kilemba, n.k. Visivyo shikana na kichwa kama mwavuli havidhuru.
  - b. Kuva nguo iloshonewa sehemu maalum ya mwili. Kwa mfano, shati, suruwali, kanzu, n.k.

### 1.5.3 Yanayokatazwa kwa mke peke yake

- Mwanamke (muhrima) peke yake anakatazwa kufanya haya mambo mawili:
  - a. Kuva niqab (vazi linalo finika uso yakabaki macho mawili).<sup>1</sup>
  - b. Kuva glovu (za mikono).

## 1.6 Mambo yasiyofaa kufanywa na muhrim/muhrima (sehemu ya 2)

- Sehemu ya pili ya mambo yasiyofaa kufanywa na muhrim au muhrima ni yale ambayo fidya yake sio fidya ya udhia. Bali inatofautiana kulingana na kosa lililofanyika kama ifuatavyo:

---

<sup>1</sup> Inaruhusiwa mwanamke aliye katika ihram kufinika uso wake asionekane na waume kwa kutumia khimar (vazi la kufinika uso) kama ilivyo katika hadithi ya Aisha mkewe Mtume.

### 1.6.1 Kuwinda wanyama wa porini

- Qur'ani imeharamisha kuwinda wanyama wote wa porini kwa lengo lolote kama chakula, michezo n.k.
- Fidya ya anaye fanya hivyo akiwa katika ihraam ni malipo ya mfano (*jazā al mithl*). K.m. muhrim akiwinda ndege, atalipa fidya ya mbuzi.

### 1.6.2 Kuingiliana na mke

- Kadhalika inaharamishwa kwa muhrim kuingiliana na mkewe. Wakionana kimwili kabla ya kumaliza amali za 'umrah, kuna mambo matatu:
  - i. Umrah inaharibika.
  - ii. Itawalazimu kufanya 'umrah ya *qadha* ambayo ihram yake ni pale pale walipohirimia 'umrah ya kwanza iliyoharibika.
  - iii. Fidya ya udhia: Kufunga siku tatu, au kulisha maskini sita, au kuchinja mnyama (mbuzi au kondoo).

### 1.6.3 Kufunga ndoa

- Mtume (sall-Allahu 'alaihi wasallam) amesema, "Muhrim haoi, haozi wala haposi,"<sup>1</sup> Kwa hivyo haifai kuposa katika hali ya ihraam, kuo, au kuoza au kushuhudia ndoa ya mtu mwengine.
- Akifanya moja ya haya, halazimiki kutoa fidya lakini uposi au ndoa iliyopitishwa haiswihi.

## 1.7 Talbiyah

- Baada ya kuingia katika ihraam, ibadah inayofuatia ni talbiya, inayoanza tangu wakati huo hadi anapoingia Masjid al-Haram kuanza twawāf.

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Muslim

- Maana ya talbiya ni kuitikia mwito, yani mwito wa Sayyidna Ibrahim ('alaihi salām) alipolingania watu kuizuru nyumba kongwa ya Makkah.
- Talbiya yenewe kama ilivyo katika Sunnah ni kusema:

---

**لَبِيكَ اللَّهُمَّ لَبِيكَ، لَبِيكَ لَا شَرِيكَ لَكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لَا شَرِيكَ لَكَ**

---

- Ni sunnah kuinua sauti kwa talbiyah kwa hadithi ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) kuwa Jibril alimwamrisha pamoja na Sahaba kuinua sauti zao kwa talbiyah.<sup>1</sup>
- Amri hii inakusanya waume na wake ispokuwa ikiwa sauti za wanawake zitakuwa fitnah mbele ya waume basi wataisoma talbiyah yao kwa sauti ya chini bila kuskika.
- Hutokea mara nyingi watu kuleta talbiya kwa sauti moja. Na hii haikupokewa katika Sunnah za Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*). Bali hadithi ya Anas katika *hijjatul wadā* inaonyesha kuwa Sahaba hawakua wakileta talbiyah zao kwa njia hizo. Kila moja wao akisema dhikri na talbiyah kwa njia yake.<sup>2</sup>

### 1.8 Tawāf

- Kuingia Msikiti mtukufu wa Makkah, amali ya kwanza ni tawāf. Kwa anayefanya *tamattu'* itaitwa *tawāf ul 'umrah*.

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Abu Daud na Tirmidhi

<sup>2</sup> Sahih Muslim



- Dua za kusoma wakati wa kuingia Masjid al Haram ni zile zile zisomwazo anapoingia nyumba yoyote ya Allah (*subhanahu wata'ala*). Akianza tawāf ndipo atakapo simamisha talbiyah kwa kuwa kwa sababu ya kuanza amali tofauti.
- Tawāf inaanzia kwenye hajar al-aswad (jiwe jeusi). Sunnah ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) ni kulishika jiwe hilo kwa mkono wa kulia na kulibusu huku ukisema: *Bismillah Allahu Akbar*.
- Ikiwa ni uzito kulishika na kulibusu kwa sababu ya wingi wa watu, atalishika kwa mkono peke yake kisha aibusu mkono huo.
- Asipoweza hivyo pia, ataashiria kwa mkono wake huku akisema *Bismillah Allahu Akbar* lakini haibusu mkono baada ya kuashiria.
- Yote haya yanafanywa kulingana na wepesi wa kutekeleza sunnah hii.



- Kinyume na wengi wanavyodhani kimakosa ikawapelekea kuingia katika udhia na madhambi kwa ajili ya kutekeleza sunnah. Katika misingi ya kiilmu, kuondoa mafsada au madhara ni aula kuliko kupatikaniwa kwa maslaha.
- Kisha anaanza tawāf kuelekea kulia akiiwacha al-Ka’bah upande wake wa kushoto.
- Akifika nguzo iitwayo *al-rukñ al-Yamāni*,<sup>1</sup> ataishika nguzo kwa mkono wake wa kulia bila ya kubusu. Iwapo hataweza, asishindane na watu wala haishirii kwa mkono.
- Bainya ya nguzo hiyo na nguzo ya hajar al-aswad atasema:

---

رَبَّنَا آتَنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

---

- Atakapofika nguzo ya hajar al-aswad atakuwa amekamilisha mzunguko mmoja wa tawāf. Ataendelea hivo hivo mpaka atimize mizunguko saba.

---

<sup>1</sup> Hii ni nguzo ilio upande wa kushoto wa hajar al-aswad

## **1.9 Mambo muhimu kuhusu Twawāf:**

### **1.9.1 Twahara**

- Tāwaf ni kama swala ispokuwa imeruhusiwa kuzungumza wakati wa kutufu.
- Kwa hivyo yaliyo shurutushwa katika sala yanashurutishwa vile vile katika Tawāf.
- Ndiposa haiswihi kwa mwanamke kutufu akiwa katika ada ya mwezi mpaka atahirike.
- Vile vile Muislamu akitangukwa na wudhu katikati ya tawāf, itambidi atoke kutawadha.
- Lakini anaporudi, je anaanza upya au ataendelea pale alipoacha kabla ya tahara kuharibika? Jibu ni ataendelea pale alipoachia tawāf yake. Kwa mfano, lau ametufu mara tatu kisha akatokwa na upepo, akirudi baada ya kutawadha atakamilisha nne zilizo salia.
- Kuna kauli ya pili ya wanazuoni katika swala hili isemayo kuwa akitangukwa na wudhu wakati wa kutufu, ataendelea na tawaf wala haimlazimu kutoka kujitahirisha. Hii inatokamana na kwamba wudhu si sharti katika twawāf bali ni sunnah.<sup>1</sup> Na huenda kauli hii ikawa ni mwafaka vile vile hasa tukizingatia uzito ulioko wa Muislamu kutoka ndani ya twawāf na kurudi namna watu walivyojaa pomoni na kusongamana.

### **1.9.2 Shaka katika idadi**

- Iwapo atakuwa na shaka katika idadi ya mizunguko, atachukua idadi ya chini iliyo ya yakini. Kwa mfano, ameingiwa na shaka, je nimetufu mizunguko minne au mitano? Atahisabu nne kwa kuwa ndio idadi ya chini iliyo na uhakika, tano ina shaka.
- Na hivi hivi ndivyo inavyo fanywa ikitokea shaka katika idadi ya raka za swala.

---

<sup>1</sup> Al-‘Uthaymeen, Majmu’ al-fatawa

### 1.9.3 Dhikri

- Hakuna dua au dhikri maalum katika mizunguko ya tawāf ispokuwa ile dua tulioitaja baina ya nguzo ya alyamāni na nguzo ya hajar al-aswad.
- Hivi basi, bora kwa Muislamu kusoma chochote anachokijua katika dhikri, k.m. sura yoyote ya Qur'an, dua, tasbih, n.k.
- Dua zilizomo katika baadhi ya vitabu za kila mzunguzko wa tawāf hazimo katika Sunnah. Muhimu ni asipoteze wakati wake katika maneno yasiyofaa ya kidunia.

## 1.10 Mambo ya sunnah katika tawāf

- Kuna mambo kadha ya Sunnah yanopendekezwa kufanywa na wanaume peke yao wakati wa tawāf:

### 1.10.1 Idhtibā'

- Maana yake ni kuva shuka (iliyo juu ya mwili) kwa kuweka bega la kulia wazi.
- Hii inafanywa kwa kuchukuwa katikati ya shuka na kuiweka chini ya kwapa la kulia na tarafu zake mbili juu ya bega la kushoto. Hii ni sunnah ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) katika *tawaf al 'umrah* peke yake, na inafanywa na wanaume katika mizunguko yote ya tawaf hiyo.



### 1.10.2 Al-Ramal

- Maana yake ni kwenda mwendo wa kasi kidogo huku ukikurubisha hatua.
- Hikma yake kama ilivyokuja katika hadith, ni kuonyesha ushujaa na nguvu ya Waislamu walipoingia Makka huku Makafiri wa Quraish wakiwasema na kuwasuta ati wamedhoofishwa na homa ya Madina. Ndipo Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) akawaamrisha watembee kwa kasi wadhihirishe kuwa wangali na nguvu.

- Hii vile vile inafanywa katika *tawaful ‘umrah* peke yake au *tawaful quduum*.

### 1.11 Swala Nyuma ya Maqam Ibrahim na Maji ya Zamzam

- Baada ya kukamilisha *tawaf al ‘umrah* mwanamume ataondoa *idhtibā’* yaani atarudisha shuka yake kama kawaida.
- Kisha ataswali rakaa mbili nyuma ya *Maqām Ibrahim* nalo ni jiwe ambalo alisimama juu yake Ibrahim (‘alaihi salām) wakati wa kuijenga al-Ka’bah.
- Sunnah ni kuswali nyuma ya *Maqām* ili iwe baina yako na al-Ka’bah. Lakini iwapo kutakuwa na zahma kubwa la watu, yaweza kuswaliwa sehemu yoyote ya Masjid al-Haram.
- Atasoma katika rakaa ya kwanza suratul Kafirun na rakaa ya pili Suratul Ikhlās (*Qul huwallahu ahad*).<sup>1</sup>
- Akimaliza kuswali, ni Sunnah kunywa maji ya zamzam. Hakuna dua maalum wakati wa kunywa maji hayo. Kisha anarudi kulishika *hajar al-aswad* ikiwa ataweza. Lau hataweza kwa sababu ya zahma, ataelekea Safā kuanza *sa’yi*.

### 1.12 Sa’y baina ya Swafā na Marwa


- Kwa anayefanya *tamattu’* hii inaitwa *sa’y al-‘umrah*. Ni sunnah anapokurubia mlima wa Swafa aseme:
- Kisha aseme: *abda-u bimā bada Allahu bihi* (naanza kwa kile alichu anza nacho Allah), yani mlima wa Swafa ambao katika aya hii ya 158, Surat-ul Baqara, umetajwa mwanzo.
- Sunnah ni kupanda kilima hicho cha Swafa<sup>2</sup> mpaka aione Al-Ka’ba, aielekee, kisha ainue mikono yake miwili kama anavyoinua akiomba dua, huku akisema dhikri ifuatayo:

---

<sup>1</sup> Sahih Muslim

<sup>2</sup> Kwa sasa hivi mlima huu umezungukwa na kizuizi haiwezekani tena kupanda juu yake. Kwa hivyo inatosha kusimama pale chini yake na kuielekea Al-Ka’bah.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لِمَلْكُ الْأَرْضِ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ  
أَنْجَزَ وَعْدَهُ وَصَدَقَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ



- Baada ya kusema hivi, aombe dua anayoitaka. Kisha aisome tena dhikri hii mara ya pili, kisha aombe dua anayoitaka. Baadaye aisome tena dhikri hii mara ya tatu halafu aondoke aelekee kilima cha Marwa.
- Kabla kufika Marwa, kuna sehemu maalum iliyo na alama ya taa za kijani ambapo ni Sunnah mwanamume kwenda kasi (kukimbia kidogo) ikiwezekana kufanya hivyo.
- Lakini ikiwa kuna msongamano wa watu, si sawa kuudhi watu kwa kuwaskuma au kuwaumiza kwa hoja ya kutekeleza Sunnah hii.
- Akifika Marwa, anafanya tena kama alivyofanya katika Swafa: Kuelekea Al-Ka'bah, kuinua mikono na kuomba kwa njia hii iliyokuja katika Sunnah.

### 1.12.1 Mambo Muhimu Kuhusu Sa'y

- ❖ Si sharti bali ni bora kwa anayefanya sa'y kuwa katika twahara. Ndio maana mwanamke katika ada yake ya mwezi aruhusiwa kufanya sa'y.
- ❖ Swala ya faradhi inapokimiwa na wakati wa kufanya sa'y, ni lazima aikate, aswali jamā'ah kisha aendelee kukamilisha sa'y wala haanzi upya.

- ❖ Hakuna dua au dhikri makhsus baina ya Swafa na Marwa ispokuwa hii dhikri tuliyo itaja hapo mbele.
- ❖ Sunnah ye kwenda kasi baina ya alama mbili za kijani ni kwa wanaume peke yao. Mwanamke au mtu anayefuatana na mwengine aliye na udhru kama mkongwe, watakiwa kutemebea kama kawaida.

### 1.13 Kunyoa au kupunguza nywele za kichwa

- Baada ya kumaliza mkondo wa mwisho wa Sa'y atatoka kupitia mlango karibu na Marwa kuelekea sehemu za kunyoa.
- Kwa kuwa *nusuk* yake ni *tamattu'* atapunguza (*taqseer*) nywele zake kwa sharti iwe ni kichwa kizima.
- Lau ingekuwa anafanya 'umrah peke yake pasina hija, basi angenyoa nywele zote kwa sababu kunyoa ni aula kuliko kupunguza. Lakini hapa katika 'umrah atapunguza kwa maana atahitaji kunyoa tena nywele wakati wa hija.
- Mwanamke naye anapunguza nywele kiasi cha kichwa cha kidole katika kila kifundo cha nywele zake. Kunyoa ni wajib katika 'umrah na ikikoseka kufanywa inalazimu fidya ya kuchinja mnyama mji wa Makka na nyama yake huganyizwa kwa maskini wa Makka.<sup>1</sup>
- Kufikia hapa atakua amemaliza ibadah yake ya umrah na ametoka katika ihraam. Sasa anaruhusiwa kufanya yote yale aliyokuwa amezuia kuyafanya wakati wa ihraam. Atasubiri hadi siku ya hija ambayo ni siku ya nane mwezi wa Dhul-hija.

---

<sup>1</sup> Sasa hivi kuna vituo makhsusi kupitia kwa serikali zinazofanya kazi ya kuchinja. Kwa hivyo Muislamu analipa tu thamani ya mbuzi au kondoo, kisha anachinjiwa.

## Sehemu ya Tatu: Utaratibu wa Kufanya Hija

### 1.14 Siku ya Nane (Yaumut-Tarwiyah)

- Hii inaitwa siku ya *tarwiyah* kwa sababu wakati huo wa zamani mahujaji walikuwa wakiteka maji watakayotumia siku za hija zinazokuja.<sup>1</sup>
- Ifikapo wakati wa *dhuhā* (kabla ya adhuhuri) siku ya nane ya Dhulhija, ataoga ikiwezekana kuoga, na kuvalaa ihraam ya haj. Hii ihraam inavaliwa pale aliposhukia (kwa mfano nyumbani au hotelini) huku akisema:

*Labbaika hajjan*      لَبَّيْكَ حَجَّاً

- Kuanzia wakati huo atakua ameingia katika ihraam ya hija na hataruhusiwa kufanya yote yaliyotajwa chini ya mlango wa ihram ya ‘umrah. Iwapo atahofia kutokee kitu huenda kikamzuia kukamilisha hija, ni vizuri kujiwekea sharti baada ya niya ya ihraam kwa kusema:

---

*Fa in habasani hābis, fa mahilli haithu habastani.*      فَإِنْ حَبَسْنَا حَابِسٌ فَمُحْلِي حِيثُ حَبَسْنَاهُ

---

- Faida ya kusema maneno haya ni kuwa lau atatokewa na jambo wakati wa ibadah yake ya hija, kwa mfano maradhi ambayo yatamzuia kukamilisha, basi atatoka katika ihram hiyo bila ya kuchinja.
- Kinyume chake ni kuwa lau hatoweka sharti hii na kukatokea kizuizi, itambidi achinje, na hii ndio maana ya ayah ya 196 ya Surat al Baqarah.
- Baada ya hapo ataaelekea Mina huku akiendelea kusema talbiyah kwa sauti. Bora iwe kabla ya saa za adhuhuri.
- Atakaa Mina siku hiyo yote pamoja na usiku wake. Swala ataziswali kwa kasru (kupunguza) bila kuchanganya. Kwa hivyo swala za dhuhri, asri, na ‘isha zote zitapunguzwa ziwe raka mbili, lakini zitaswaliwa kwa wakati wake. Hakuna swala zengine za sunnah zinazoswaliwa hapa ispokuwa sunnah ya alfajiri na witri.

---

<sup>1</sup> Al-Mughni, Ibn Qudamah: uk. 205

- Atalala hapo Mina (*mabit*) hadi alfajiri. Ataiswali swala ya fajri hapo Mina siku ya pili (ya tisa). Jua likishachomoza, ataanza kuelekea Arafat.

### 1.15 Siku ya Tisa (Yaumu 'Arafah)

- Ni bora kufika uwanja wa Arafah asubuhi ya tisa ya Dhulhija, kabla ya adhuhuri.
- Kufika hapo, ni sunnah kuswali katika mskiti wa Namira, hapo Arafah, swala ya adhuhuri na asri kwa kukusuru na kuchanganya wakati wa adhuhuri (*jam'u taqdeem*) na kuskiliza mawaidha au khutbah ya imam siku hiyo ikiwezekana.
- Hapo ndipo aliposimama Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) kuhutubu khutbah yake ya mwisho.
- Ikiwa haikuwezekana kwa sababu ya msongamano mkubwa wa watu, ataswali katika hema au pahali popote kwa jama'ah.
- Baada ya hapo, atasimama katika jangwa la Arafah na sunnah ni kusimama kuelekea kibla na kuomba. Inajuzu kusimama popote madamu uko katika jangwa hilo kwani Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) amesema, “Nimesimama hapa, (lakini) Arafah yote ni sehemu ya kusimama.”<sup>1</sup>
- Mahujaji watakiwa kuwepo hapo siku hiyo yote, wasiondoke mpaka jua lizame wakati wa magharibi.
- Jua likishazama ndio wanafaa kuondoka kuelekea Muzdalifah. Muda huu wote atakiwa Muislamu ajishughulishe na dhikri na dua.
- Miongoni mwa dhikri zinazo tajwa katika siku hii ni hadithi hii: “Dua bora ni dua ya siku ya Arafah, na bora ya maneno niliosema mimi na Manabi wengine kabla yangu ni: “*La ilaha illallahu wahdahu la sharika lahu la mulku walahu hamdu wahuwwa 'ala kulli shai in Qadeer.*”<sup>2</sup>

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Muslim

<sup>2</sup> Imepokewa na Tirmidhi na As-hab al-Sunan

### 1.15.1 Baadhi ya Makosa yanofanyika Siku ya Arafah

- ❖ Kosa kubwa la hatari huenda likatokea siku hii ni mahujaji kukaa nje ya mipaka ya Arafah wakidhani kuwa wako Arafah. Serikali ya Suudia imerahisisha kujua mipaka hio kwa kuweka alama za wazi kuonyesha mwanzo na mwisho wa kila kituo. Hivi basi, anayebakia nje ya Arafah muda wote huu, mpaka kuingia magharibi huwa ameikosa *wuqūf* na Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) amesema: *Hija ni ‘Arafah.*<sup>1</sup>
- ❖ Kosa lengine ni watu kuomba kwa kuelekea mlima wa Arafah badili ya kuelekea kibla. Kwa baadhi ya watu, jabali hili ambalo watu huliita *jabal-al rahmah*<sup>2</sup>, una utukufu au fadhla fulani. Ndiposa utawaona wanaji shughulisha sana na huu mlima, wengine wakiupanda mpaka juu. Yote haya hayana asli katika mafundisho ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*).
- ❖ Kuondoka Arafah kabla ya kuingia magharibi. Hii ni kinyume na maagizo ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) kama ilivyo katika hadith ya Jaber. Sunnah ni kusubiri hadi jua lizame ndio ipatikaniwe fadhla kamili ya *wuqūf*.
- ❖ Kufunga: Hapana shaka siku hii ni tukufu na imekuja katika sunnah ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) fadhla ya kufunga siku ya Arafah. Lakini hii ni kwa asiyekuwa katika ibadah ya hija. Ama yule aliye katika ibadah ya hija, si sunnah kwake kufunga, na kufanya hivo ni kunyume na mafundisho ya Mtume wetu (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*).

### 1.16 Kulala Muzdalifah

- Kutoka Arafah, mahujaji watakiwa kuelekea Muzdalifah kwa upole na utulivu huku wakiendelea kuleta talbiya na dhikri zengine kama takbir.
- Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) aliwahimiza Sahaba kuwa na utulivu akisema: “*Al-Sakinah, al-Sakinah*” (Kueni na utulivu! Kueni na utulivu).<sup>3</sup>
- Sunnah ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) ni kuichelewesha swala ya maghrib hadi kufika Muzdalifa ndipo aliamrisha swala ya maghrib iadhiniwe na ikimiwe wakaswali. Baada ya watu kuweka mizigo yao,

---

<sup>1</sup> Imepokewa na Abu Daud na Tirmidhi

<sup>2</sup> Jina hili halina asli au ushahidi katika mafundisho ya Sunnah

<sup>3</sup> Imepokewa na Muslim

akaamrisha ikimiwe sala ya isha, wakaswali isha.<sup>1</sup> Kisha akalala hapo Muzdalifah usiku huo.

- Kwa hivyo, amali muhimu iliyoko Muzdalifa baada ya swala ni kulala na kupumzika ili aendelee na amali ya hija bila uzito.
- Baadhi ya watu huenda kinyume na mafundisho haya kwa kukesha usiku huo kwa ibadha au katika mazungumzo yasiyokuwa na maana.
- Ifikapo alfajiri, atakiwa asimame kuswali na jama'ah kisha asimame hapo aombe Mungu kuelekea kibla hadi kabla kuchomoza kwa juu. Baada ya hapo mahujaji waelekea Mina.

### 1.17 Ruhusa kuondoka Muzdalifa kabla ya alfajiri

- Kwa wale walio na udhaifu kama wanawake, watoto na wagonjwa, wameruhusiwa kuondoka Muzdalifa kabla ya alfajiri lakini baada ya nusu ya usiku.<sup>2</sup>
- Na wale wanaofuatana nao pia mionganini mwa watu walio na nguvu zao wanaruhusiwa kuondoka wakati huo kuelekea Mina. Wakifika Mina watarusha mawe katika nguzo (*jamrah*) ya 'aqabah hata ikiwa ni usiku au baada ya alfajiri.

### 1.18 Kuokota vijiwe

- Vijiwe vya kurusha katika *jamarah* vinaweza kuchkuliwa hapo Muzdalifah. Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) alimwamrisha mtoto wa ami yake, Al-Fadhl bin 'Abbas amuokotee vijiwe saba peke yake.<sup>3</sup>
- Kwa hivyo si lazima kuchukuwa vijiwe vyote vya kurusha (70) hapo muzdalifa, bali unaweza kuchukuwa pahali popote hata Mina.



<sup>1</sup> Abu Daud na Ibn Majah

<sup>2</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim


<sup>3</sup> Sahih Muslim

- Ukubwa wa kijiwe kimoja ni kiasi cha tembe ya haragwe au karibu na hapo – si kubwa sana wala ndogo sana. Ni kiasi ambacho kinaweza kurushwa kwa ncha za vidole peke yake, wala haihitajii kurushwa kutumia kiganja kizima cha mkono. Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) akahimiza watu kurusha kwa mfano wa vijiwe kama hivyo na akakataza *ghuluw*, yaani kuongeza na kuvuka mipaka.<sup>1</sup>

## 1.19 Siku ya Kumi (Yaumun Nahri)

Wanapofika mahujaji Mina kuna amali nne watakiwa kuzifanya siku hiyo:

### 1.19.1 Kurusha vijiwe (*Ramyu*)



- Hii ndio amali ya kwanza ya mahujaji wafikapo Mina siku ya kumi, ambayo ndio siku ya ‘idi.
- Hapa ndio mwisho wa kuleta talbiya ambayo alikuwa akiisema muda wote tangu kuingia katika ihraam ya hija.
- Sunnah ni kufanya *ramyu* baada ya kuchomoza kwa kujua.

---

<sup>1</sup> Sahih Muslim

- Tumekwisha kutaja kuwa wale walio na udhru wanaruhusiwa kurusha kabla ya kuchomoza jua, bora iwe ni baada ya nusu ya usiku.
- *Jamrah* hapa ni ya *al-'aqabah* iliyo karibu na Makkah. Idadi ya vijiwe vinavyo rushwa ni saba.
- Atainua mkono wake wa kulia (ikiwezekana) kwa kila kijiwe huku ukisema: *Allahu akbar*.
- Lazima kila kijiwe kianguke ndani ya shimo la *jamrah*. Lau atarusha vijiwe vyote kwa pamoja, itahisabika ni kijiwe kimoja peke yake atabaki na visita. Na lau kijiwe kitapija *jamrah* kitoke nje, hakitahesabiwa katika idadi ya vijiwe saba.
- Pia ni bora kurusha vijiwe hivyo huku Mina iko upande wake wa kulia na Makka upande wa kushoto. Ingawaje hili linaweza kuwa vigumu kutekeleza hasa kwa kuwa watu ni wengi. Hivi basi, atarusha vijiwe kwa upande wowote amba ni sahali kwake.
- Ikitokea shaka katika idadi ya vijiwe (kwa yule aliyebeba vijiwe zaidi ya saba), atarudi katika idadi ya chini. K.m., akishuku je, nimerusha vijiwe sita au saba, atahisabu vijiwe sita, kwa kuwa ndio idadi iliyo ya yakini. Wakati wa mwisho wa kurusha vijiwe katika *jamrah* hili ni alfajiri ya siku ya kumi na moja ya Dhul- hija.

#### *1.19.1.1 Baadhi ya makosa katika ramyu al-jamrah*

- ❖ Kufanya ghuluw (upitaji wa mpaka) katika kurusha vijiwe inayowapelekea watu wengine kurusha yasofaa kurushwa kama viatu, vitambaa n.k.
- ❖ Kuitakidi kuwa shetani yupo katika ile nguzo inayopigwa mawe na huu ni ujinga. Lengo la lile nguzo kuweko (*shākhīs*) ni kuhakikisha kuwa kijiwe kimeingia ndani ya lile shimo. Wengine hata husema tunapiga shetani, na hii pia si sawa kwani kurusha vijiwe ni ibadah mionganoni mwa ibadah zilizo amrishwa kutajwa Mwenyezi Mungu ndani yake, sio makhsus ya kupiga shetani.
- ❖ Kuwakilisha mtu mwengine kwa amali hii. Ikiwa ni kwa udhru kama udhaifu, uzee au maradhi, haina neno. Lakini pasina udhru, bali yule aliywakilisha ana uwezo, basi ni makosa.

- ❖ Kuwacha kusema takbir ambayo ni Sunnah iliyo thubutu kwa kila kijiwe kinacho rushwa na badala yake kusema maneno yasio na msingi wala maana, kama kumlani shetani n.k.

### 1.19.2 Kuchinja (*al-Nahr*)

- Amali ya pili inayofanywa siku hii ya kumi ni kuchinja mnyama.<sup>1</sup>
- Hii ni wajib kwa anayefanya nusuk ya *tamattu'* na *qirān* sio kwa anayefanya *ifrād*.
- Wakati wa kuchinja ni kuanzia siku hio ya ‘idi hadi kuzama kwa jua siku ya mwisho katika siku za *tashreeq*,<sup>2</sup> (ambayo ni tarehe 13). Inaruhusiwa pia kuchinja nyakati za usiku wa masiku hayo.
- Kwa asiyé na uwezo wa kuchinja ilhali ni *mutamatti'* au *qaarin*, itambidi afunge siku kumi. Tatú katika hizo ndani ya siku za hija, ima kabla ya siku hii ya ‘idi, au katika siku tatu za *tashreeq*.<sup>3</sup> Saba zinazobaki atazifunga atakapo rudi kwao nyumbani kama ilivyo katika aya ya 196 ya Surat al-Baqarah.

### 1.19.3 Kunyoa au Kupunguza

- Amali ya tatu inayo fanywa siku hii ni kunyoa nywele zote za kichwa (kwa manamume peke yake) au kuzipunguza.
- Hapa kunyoa nywele zote ni bora kuliko kupunzua kutokana na dua ya Mtume (*sall-Allahu 'alaihi wasallam*) alipo waombea wanaonyoa nywele zao zote mara tatu ilhali wale wanaopunguza aliwaombea mara moja pekee.<sup>4</sup>
- Na sunnah wakati wa kunyoa ni kuanza upande wa kulia wa kichwa kisha upande wa kushoto kama ilivyo katika hadith ya Anas (*radhi Allahu 'anh*).<sup>5</sup>

---

<sup>1</sup> Kuchinja siku hizi inafanywa na wakala mbali mbali zilizo afikiwa na serikali kwa kurahisisha kazi hiyo.

<sup>2</sup> Siku za *tashreeq* ni siku ya 11, 12 na 13 Dhulhijjah.

<sup>3</sup> Na hii ndio hali ya pekee inayo ruhusiwa mtu kufunga siku za *tashreeq*

<sup>4</sup> Imepokewa na Bukhari na Muslim

<sup>5</sup> Imepokewa na Muslim

#### 1.19.4 Twawāf al-ifādha

- Akimaliza hapo, atarudi Makka kufanya twawāf ambayo ni nguzo katika hija, pia inaitwa twawāf al-hija na twawāf al-ziyāra.
- Katika twawāf hii, hakuna *ramal* wala *idhtibā* ambazo zilikuwa ni sunnah katika twawāf ya ‘umrah.
- Baada ya kutufu mizunguko saba ataswali sunnah ya twawāf nyuma ya *Maqām Ibrahim* akiweza. Kama hakuweza basi sehemu yoyote ya Masjid al-Harām.

#### 1.19.5 Sa’iy al-Hija

- Amali ya mwisho katika siku hii ni sa’iy ambayo inafanywa baada ya twawāf na kuswali nyuma ya *Maqām*. Wakati wa sa’iy pia unaendelea hadi mwisho wa mwezi wa Dhul-hija.

### 1.20 Utaratibu wa Amali Siku ya Kumi

- Utaratibu huu tulio utaja ndio unaotakiwa kufatwa katika siku hii ya kumi ya Dhul-hijja.
- Lakini kwa sababu ya uzito, zahma, na misongamano ya watu wengi, inafaa kutanguliza amali moja kabla ya nyengine. K.m. kunyoa nywele kabla ya kutufu, au kuchinja kabla ya kunyoa n.k. Asli ya ruhusa hii ni kauli mashuhuri ya Mtume (*sall-Allahu ‘alaihi wasallam*) katika siku hii: “*If’al walā haraj*” (fanya wala hakuna ubaya).<sup>1</sup>
- Hii inaonyesha wepesi na usahali wa dini hii hasa katika nyakati au hali ambazo ibadah huenda zikawa nzito kwa sababu tofauti tofauti, pamoja na kwamba Muislamu amehimizwa kuwa na subra.

### 1.21 Kutoka katika ihraam (*Tahāllu*)


- Siku hii vile vile mwenye kuhiji hutoka katika ihram yake, akaruhusiwa kufanya yaliyokuwa yameharamishwa kwake kuyafanya. Hii inaitwa *tahallul* ambayo imegawanyika sehemu mbili:

---

<sup>1</sup> Bukhari na Muslim


### 1.21.1 Tahallul Ndogo

- Imeitwa ndogo kwa sababu inahalalisha kila kitu baada ya *ihraam* ispokuwa kuingiliana na mke.
- *Tahallul* hii inapatkaniwa kwa kufanya mawili katika ya haya mambo matatu:



### 1.21.2 Tahallul kubwa

- Imeitwa *tahallul* kubwa kwa sababu inahalalisha kila kitu mpaka kuingiliana na mke.
- Hii *tahallul* inapatkaniwa kwa kufanya ile itakayo bakia katika *tahallul* ndogo pamoja na *sa'y ya hija* (kwa mwenye kufanya *tamattu*).



### 1.22 Siku za Tashreeq.

- Hizi ni siku za 11, 12, na 13 za mwezi wa Dhulhijja. Zimeitwa tashreeq kwa kuwa siku hizo watu walikuwa wakianika nyama za udh-hiya juani mpaka zikauke.
- Na ndizo siku zilizotajwa katika aya 203 ya Surat al-Baqarah:

### 1.23 Kurusha Vijiwe (Ramyu)

- Katika jumla ya kumtaja Mwenyezi Mungu ndani ya siku hizi ni kurusha vijiwe Mina.
- 



- Amali hii inaanza baada ya kupenduka kwa jua (*zawāl*) hadi kuanguka kwa jua (magharibi).
- Wale walio na udhru kama wazee na madhaifu wasioweza kurusha wakati wa msongamano, wameruhusiwa kusubiri hadi saa za usiku. Na kwa sababu wakati wa kurusha umewekwa wa kutosha, hakuna haja ya misongamano au fujo, bali aula ni kusuburi zile saa ambazo zahma litakua limepungua na kuanza ibadah ya ramyu.
- Jinsi ya kurusha kama ilivyo bainishwa katika sunnah ni kuanza na *al-jamrat al-ūlā* iliyo ya mwisho kabisa kutoka Makka na ya kwanza kutoka Mina.
- Atasimama kuelekea qibla (akiweza) arushe vijiwe saba, akisema *Allahu akbar* kila mrusho.
- Kisha atasongea sehemu kando isiyofikiwa na vijiwe, asimame hapo aombe kwa muda mrefu akielekea qibla.<sup>1</sup>
- Baadaye aje katika *jamrah* ya pili au ya katikati, arushe vijiwe saba, na asimame aombe kuelekea qibla kama alivyofanya mwanzo.

<sup>1</sup> Ibnu udaamah, Al-Mughni.

- Akimaliza, atakwenda katika *jamratul kubra* iliyo karibu na Makka. Atarusha vijiwe saba hapo huku Makka iko upande wake wa kushoto (ikiwezekana) kisha ataondoka (haombi baada ya *jamrah al-'aqabah*).

### 1.24 Kulala Mina

- Hii ni moja wa mambo ya wajib katika Hija. Inawalazimu mahujaji kulala Mina (baada ya siku ya 'idi), siku ya 11 na 12 kwa yule aliye na haraka, au 11, 12 na 13 kwa yule atakayekamilisha.
- Kwa yule aliye na haraka (*muta'ajjil*), atarusha vijiwe siku ya 11 na 12 peke yake, kisha aondoke Mina siku hiyo ya 12 **kabla** ya jua kuzama (magharibi).
- Ikiingia magharibi ilhali bado yuko Mina, itambidi akamilishe siku ya 13.
- Kwa yule atakaye kamilisha hadi tarehe 13, ataendelea kurusha vijiwe siku ya 13 baada ya *zawaal*.<sup>1</sup> Na huyu bila shaka ndiye aliye bora katika fadhla na ndivyo alivyo fanya Mtume (*salla-Allahu 'alaihi wasallam*).
- Akiwa Mina, ataswali swala zote tano kwa *kasru* (kupunguza) bila ya *jam'u* (kuchanganya).
- Baada ya kila swala mahujaji wataleta takbir baada ya kila swala ya faradhi inaposwaliwa jama'ah. Hii inaitwa *takbeer muqayyad*, na inaanzia siku ya 'idi baada ya adhuhuri hadi swala ya 'asri siku ya kumi na tatu.<sup>2</sup>

### 1.25 Twawāf al-Wadaa'

- Anapoazimia kufunga safari ya kurudi nyumbani, atafanya twawāf ya mwisho ya kuaga, ambayo ni mionganini mwa mambo ya wajib katika hija.
- Amri ya Mtume ((*salla-Allahu 'alaihi wasallam*) ni kuifanya Ka'bah kuwa ndio pahali pa mwisho pa kuondokea na kuaga Makka.<sup>3</sup>

---

<sup>1</sup> Wakati wa adhuhuri baada ya jua kupindukia upande wa pili wa dunia.

<sup>2</sup> Kwa wasiokuwa mahujaji, takbir zao zinaanza tangu alfajiri ya siku ya Arafa na kumalizika alasiri ya siku 13.

<sup>3</sup> Imepokewa na Muslim

- Inafanywa kama twawāf nyengine ya kawaida lakini bila ya *ramal* (kuenda haraka), wala hakuna *idhtibā* kwa wanaume kwa sababu mahujaji watakuwa tayari wametoa ihraam zao na kuvaan nguo za kawaida.
- Mwanamke aliye na udhru wa hedhi au uzazi (*nifās*) hawajibiki kufanya twawāf hii kwa hadith ya Ibn ‘Abbas kuwa mwanamke aliye na hedhi amekhafifishiwa.
- Inaruhusiwa pia kuichelewesha twawāf ya *ifādha* na kufanya wakati wa kabla ya safari. Akifanya hivyo itakua imetosha wala hakuna haja ya kufanya twawāf al-wadā baada ya hapo, kwa sababu lengo la kufanya al-Ka’ba kuwa kituo cha mwisho kimepatikaniwa.

### 1.25.1 Baadhi ya Makosa Katika Twawāf al-Wadā

- ❖ Kubakia Makka baada ya twawāf al-wadā kwa lengo kama kufanya biashara au kulala hapo. Akifanya hivi, itambidi arudie tena hiyo twawāf. Lakini akibaki hapo kwa muda wa masaa kadha ili kujitayarisha na kufunga mizigo, hawajibiki kurudia kwa sababu tayari amejiandaa kwa safari.
- ❖ Kufanya *sa'y* baada ya twawāf al-wadā.
- ❖ Kutoka Masjid al-Haram baada ya wadā kinyumanyuma au kisogosogo kwa kuitakidi kuwa haifai kuipa al-Ka’ba kisogo wakati wa kutoka. Na ikitadi hii haina msingi wowote.

### 1.26 Kwenda Madina

- Kufikia hapa mahujaji watakuwa wamemaliza ibada yao ya hija na ‘umrah. Mola (*subhanahu wata'ala*) awakubalie ibda hizo.
- Kwa yule aliyeingia Makka moja kwa moja kuanza ‘umrah, ni vizuri kufunga safari kusali al-Masjid al-Nabawi, Madina. Niya yake iwe ni ziyara ya mskiti wa Mtume Madina wala siyo ziyara ya kaburi lake na makaburi ya masahaba, kwa ushahidi wa hadithi inayokataza Muislamu asifunge safari ispokuwa kwa miskiti mitatu: (msikiti wa Makka, msikiti wa Madina na Bait al-Maqdis).<sup>1</sup>

---

<sup>1</sup> Sahih al-Bukhari

- Ikiwa ashafanya ziyara ya Madina, ataelekea nyumbani moja kwa moja baada ya kuaga mji mtukufu wa Makkah.